LAND DEVELOPMENT & GOVERNANCE INSTITUTE

Empowering Society

TATHMINI YA SEKTA YA ARDHI: AWAMU YA 16

UWEPO WA UTASHI WA KISIASA NA USAIDIZI KUTOKA KWA WADAU NI MUHIMU KWA MAREKEBISHO KATIKA SEKTA YA ARDHI

Matukio ya hivi maajuzi katika sekta ya ardhi ni sabau nzuri ya kutumaini. baada ya tume ya ardhi kuahirisha kesi mbele ya mahakama ya juu zaidi kufuatia malumbano baina ya tume hiyo na wizara ya ardhi, nyumba na ustawishaji wa maeneo ya mijini. Mahakama hiyo ilizipa taasisi hizo mbili muhimu muda wa miezi mitatu ili kutatua tofauti zao la sivyo warejee mahakamani kwa uamuzi.

Uamuzi huu ulifwatiwa kwa karibu na ushauri kutoka ngazi za juu baada ya rais na naibu wake kuongoza makubaliano baina ya tume na wizara hizo husika. Makubaliano hayo yaliwashurutisha kufanya kazi kwa ushirikiano. Japo makubaliano hayo hayajafikia umma, ni matumaini ya wengi kwamba wahusika hao wataweza kushirikiana na kuwajibika kwa pamoja ili kutekeleza wajibu wao, jambo ambalo linapaniwa kuwa hatua muhimu zaidi katika mipango ya ardhi na utoaji wa huduma.

Wadau pia wamehoji kuwa wapo tayari kusaidia utekelezaji wa marekebisho ya ardhi na ulainishaji wa mipango japo taasisi hizi mbili zinapaswa kutoa mwongozo bora kwa kushirikiana na kukutana mara kwa mara. Haya yalijiri katika warsha wa hali ya juu uliyoandaliwa na Taasisi ya Uendeleshaji na Usimamizi wa Ardhi katika hoteli ya Sarova Panafric Jumatano tarehe 26 Novemba 2014. Warsha hiyo iliwaleta pamoja wadau mbali mbali wakiwemo, wizara na tume ya ardhi, tume ya utekelezaji wa katiba cic, kamati husika kutoka bunge la kitaifa na seneti, wizara zingine husika, serikali za kaunti, kitengo cha sheria, sekta ya kibinafsi, taasisi za utafiti na mafunzo, vyama vya kitaaluma, taasisi za kidini, Baraza la Kitaifa la Wazee, wana habari, na vyama vya kijamii.

Lilikuwa tukio la kihistoria kuona waziri wa ardhi na mweneyekiti wa tume ya ardhi kuhudhuria kwa mapoja warsha hiyo na ni jambo linalostahili kutungwa mkono na kupongezwa. Wawili hao waliongeza matumaini ya wadau walipokiri kuwa makubaliano yaliyoongozwa na rais yanaendelea vyema na kamati ya kiufundi iliyobuniwa wakati huo tayari imewasilisha ripoti yake. Baada ya kupitishwa, ripoti hiyo inayolenga kufafanua majukumu ya kimsingi itakabidhiwa mahakama ya juu zaidi na itasaidi kuimarisha uhusiano wa taasisis hizo mbili.

Hivyo basi Wizara na Tume ya Ardhi zinapaswa kuzingatia utashi uliopo kuendeleza mipango katika sekta ya ardhi. Wawili hao pia wanafaa kuimarisha mipango ifuatayo:

1. kufikisha tamati sheria na marekebisho yaliyosimama:

Wizara ya ardhi na tume husika zinapaswa kushirikiana na wizara zingine husika sawa na vitengo vya serikalini na bunge kujadili na kupitisha sheria hizi:-

- Mswada uhusianao na Ardhi ya Umma (Kipengee 63 cha katiba),
- Merekebisho ya Sheria za Ardhi, Usajili wa Ardhi na Tume ya Ardhi
- Sheria zingine za kusaidia utekelezaji wa Sheria za Ardhi, Uandikishaji wa Ardhi na Tume ya Kitaifa ya Ardhi Mswada unaohusiana na Miondombinu,
- Mswada wa Ufurushaji na Utoaji wa Makao Mbadala,
- Sheria zilizorekebishwa zinazohusiana na Matumizi ya Ardhi (Kipengee 63 (b) cha Katiba),
- Sheria zihusianazo na Maliasili (Kipengee cha 71 cha Katiba),
- Sheria zihusianazo na Mazingira (Kipengee cha 72 cha Katiba),
- Sheria ya Kutatatua Mizozo na Dhuluma za Miaka ya Awali (chini ya Sheria ya Tume ya Ardhi)

2. Utoaji wa hati miliki za ardhi/kutamatisha mipango ya hati miliki iliyokwama:

Bado kuna mipango kadha wa kadha iliyolemaa, hii ni pamoja na kutenga maeneo maalumu ya matumizi ya ardhi, ugawanyaji wa vipande vya ardhi hususan vile vya kampuni kubwa kubwa na vyama vya ushirika, na mashamba makubwa chini ya mipango ya ugawaji au utoaji wa makao katika maeneo ya mjini. Hatua hizi zinapaswa kuharakishwa. Jamii zinazozingatia kubadili mashamba yao na kuwa ya kibinafsi zinapaswa kusaidiwa pindi tu sheria ya ardhi ya kijamii itakapotekelezwa. Haya yatasaidia wakenya wengi kupata hati miliki za ardhi na kutoa hisia ya umiliki wa vipande vyao vya ardhi, hii itapunguza mizozo ya ardhi na kusaidia kuimarisha uchumi wetu.

Wakati wa warsha hiyo waziri alihoji kuwa takriban hati miliki laki mbili zitatolewa kwa wakaazi wa kaunti ya Meru. Ikizingatiwa kuwa baadhi ya maeneo maalum yanayopaswa kutengwa bado hayajashughulikwa tangu taifa hili kujinyakulia uhuru ndio maana taasisi hii inashauri kuwa utoaji wa hati miliki ufanyike kwa haraka na uzingatiwe kama jambo muhimu wa kitaifa. Hasara ipatikanayo kutokana na kuchelewa huku ni kubwa sana kwa wananchi sawa na taifa zima.

3. Uboreshaji na Ustawishaji wa mfumo wa habari na usimamzizi wa ardhi:

Wizara ya ardhi inapaswa kuboresha rekodi na mipango yake kwa kutumia teknolojia ya kisasa, na kubuni mfumo imara wa habari na usimamizi wa ardhi. Haya yatahitaji kuhifadhi rekodi za sasa za umiliki wa ardhi sawa na ramani kwa misingi ya kidijitali. Japo hatua nizi zitagharimu kiasi kikubwa cha fedha na huenda ikachukua muda mrefu kustawisha, ndio njia mwafaka ya kuboresha rekodi za ardhi sawa na usimamizi wa sekta ya ardhi. Hii itakabili changamoto ya ufisadi katika utoaji wa huduma, na pia itaboresha mapato yatokanayo na sekta hii kote nchini. Serikali za kitaifa sawa na zile za kaunti zinapaswa kuzingatia ustawishaji wa mfumo wa haina hii. Japo waziri alikiri kuwa hatua zinaendelea kuchukuliwa, ni vyema iwapo angeeleza njia wanayopania kutumia ili kustawisha mifumo ya kitaifa ya utoaji habari na usimamizi wa ardhi na kufafanua majukumu ya wadau mbali mbali wanaohusika katika kila ngazi.

4. Ustawishaji wa mbinu ya kuwahusisha wadau

Ili kufaidi vyeam kutoka kwa utahi uliopo kwa sasa, (kutoka kwa wizara husika, sekta ya kibinasfi, vyama vya kijamii na mashiriki wa kimaendeleo) wizara na tume ya ardhi zinapaswa kubuni mbinu ya kuwahusisha wadao mbali mbali. Japo waziri na mwenyekiti wa tume ya ardhi walikubaliana na mabo haya kwa kikamilifu, ni vyema wawili hao watoe mwongozo mwema ili mambo muhimu yahusianayo na mipango hii yatekelezwe haraka iwezekanavyo.

Imetayarishwa na Taasisi ya Uendeleshaji na Usimamizi wa Ardhi tarehe 2 Desemba 2014